

LUDEWA



YETU

Karibu Ludewa kwa uwekezaji.

1. Kilimo
2. Mifugo
3. Madini
4. Misitu
5. Utalii

HABARI

www.ludewadc.com

Novemba 2022



Ujenzi wa Jengo la Utawala Waendelea



Tangu kuanzishwa kwa Halmashari ya Wilaya ya Ludewa mwaka 1975 haijawahi jenga jengo la kiwango kama hili ila chini ya kipindi cha uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan Wilaya ya Ludewa imepatiwa fedha za ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri inayoendelea na ujenzi hadi kukamilika kwake mwaka 2023.

Ikumbukwe ya kwamba fedha ya utekelezaji wa mradi huo Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari imetoa yote na ujenzi wa jengo hilo unaendelea kwa kasi na inakadiliwa Februari 2023 litaanza kutumika.

Kwa kipindi cha mwaka 2020/2021 Halmashauri ilipoke Milioni 750 na kipindi cha pili Halmashauri ilipokea Bilioni 1 na kwa kipindi cha tatu cha mwaka 2022/2023 tImepokea Milioni 900 ambapo ukamilikaji wa jengo hili litakuwa limekamilika kwa ghalama za jumla za shilingi Bilioni 2.8

Ipo miradi mingi inayotekelezwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa na yote inaendelea kwa kasi.

Katika kipindi cha Mwaka fedha 2021/2022 iliidhinishiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutumia shilingi 10,461,729,310.47 kwaajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

Kwa kipindi cha Mwaka 2021/2022 ime-tekelezwa miradi mbalimbali kwenye Wilaya ya Ludewa, Ujenzi wa Zahanati na ukamilishaji wa Zahanati kwenye Kata mbalimbali, Ujenzi wa Maabara kwa shule za Sekondari zaidi ya 4, na zaidi ya shule 14 zimefikiwa kwa kutekeleza kazi ya ujenzi lakini pia ukamilishwaji wa madarasa kwa shule za Msingi na Sekondari.

Kwa namna ya kipekee tunakila sababu ya kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwakuendelea kuijenga Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan hakutuacha nyuma wananchi wa Wilaya ya Ludewa, kwa mwaka 2021/2022 alitupatia fedha kwaajili kutekeleza miradi mbalimbali kwa fedha ya Uviko 19, na moja ya mradi uliotekelezwa

ni pamoja na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU) katika Hospitali ya Wilaya ya Ludewa ambapo kiashi cha shilingi 250,000,000 zimekamilisha jengo hilo.

Na zaidi ya matundu 60 ya vyoo yamejengwa katika shule mbalimbali za Wilaya ya Ludewa ikiwemo shule ya sekondari Mavanga ambapo ilipataiwa fedha ya kujenga matundu 12.

FEDHA ZA TASAF

Naam hapa utaona ni kwanamna gani wadau mbalimbali jinsi wanavyo shiriki kikamilifu shughuli za maendeleo kwenye Halmashauri yetu ya Wilaya ya Ludewa.

Ipo miradi mbalimbali iliyotekelezwa na fedha za TASAF 2021/2022 ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye maeneo mbalimbali kwenye halmashauri yetu ya wilaya ya Ludewa kishi cha Sh. 329,701,074,503 zimefanikisha kutekeleza miradi yaki-maendeleo.

Ipo miradi iliyotekelezwa kwenyemaeneo yote ya Wilaya ya Ludewa kwa kila kata kukuta na sehemu ya gawio la utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao ikiwa ni pamoja na kutekelezwa kwa miradi ya fedha za Ruzuku (SEQUIP) 2021/2022, Utekelezaji wa miradi ya kupambana na UVIKO 19 kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Kwakuongezea nikuhamasishe kuendelea kutembelea mitandao yetu ya kijamii huko utaziona picha za miradi yote inayotekelezwa. Facebook na You Tube, @LUDEWA DC, Instagram, Twitter na Tiktok, @HLudewa na tovuti ni www.ludewadc.go.tz

Sambamba na utekelezaji wa miradi mbalimba serikali haija waacha nyumba wananchi kwa kuwapa sehemu ya makusanyo ya mapato ya ndani.